USAID
KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

TZ21
21ST CENTURY BASIC EDUCATION PROGRAM

PROGRAMU YA ELIMU YA MSINGI YA TZ21

# MWONGOZO WA MAFUNZO YA KUIMARISHA KUSOMA KATIKA MTAALA



**PROGRAMU YA ELIMU YA MSINGI YA TZ21**

# MWONGOZO WA MAFUNZO YA KUIMARISHA KUSOMA KATIKA MTAALA

**MACHI 2015**

## Shukrani

Mafunzo haya ya Kuimarisha Usomaji katika Mtaala kwa walimu wa darasa 3 na 4 ni matokeo ya msaada wa watu wa Amerika kupitia ufadhili wa Shirika la Misaada ya Kimataifa ya Mendeleo la Marekani (USAID) kwa Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21. Msaada huu wa watu wa Marekani unalenga kujenga uwezo wa watoto wa Tanzania kielimu. Msaada huu unakusudia kuboresha stadi za usomaji za wanafunzi katika hatua za awali wanapoanza kusoma shuleni ili kuinua matokeo mazuri ya usomaji yanayotarajiwa kwa watoto wote wa shule za Mtwara na Zanzibar. Programu ya Elimu ya Msingi ya TZ21 inatambua mchango wa kipekee uliotolewa na Amy Pallangyo-Mtaalam Mshauri wa TZ21 katika kutayarisha mwongozo huu wa mafunzo. Pia shukrani ziwaendee wafanyakazi wataalamu wa TZ21 na MOEVT kwa kuendesha mafunzo kwa wawezeshaji wa mafunzo ngazi ya wilaya kwa mkoa wa Mtwara na Zanzibar.

Hivyo basi shukrani za pekee zinatolewa kwa Shirika la Misaada ya Kimataifa ya Mendeleo la Marakani (USAID) kwa kufadhili kazi hii.

Maoni yaliyomo katika mwongozo huu ni ya waandishi. Hayawakilishi kwa namna yoyote ile maoni au msimamo wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) au Serikali ya Marekani (USA).

Kimetolewa na kuchapishwa kwa ufadhili wa UASID wa Programu ya Elimu ya Msingi (TZ21) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Tanzania Bara na Zanzibar

## Malengo

Walimu waweze:

1. Kutafakari kuhusu maendeleo na changamoto za kusoma, kuandika na kutumia msamiati kujifunza maudhui ya masomo mengine darasani.
2. Kujifunza zaidi jinsi ya kupambana na changamoto za ufundishaji zinazowakabili.
3. Kujifunza na kufanyia mazoezi mbinu mpya za kusoma, kuandika na kutumia msamiati katika kujifunza maudhui ya masomo mengine.
4. Kuchunguza dhana ya matini inayoendana na ngazi/uwezo wa msomaji.
5. Kuandika matini mpya za kufundishia katika ngazi mbalimbali kulingana na mahitaji tofauti tofauti ya kujifunza.
6. Kutumia matini mpya kuandaa masomo ya kufundisha maudhui kwa kutumia mbinu za kusoma, kuandika na msamiati.

## Yaliyomo ukurasa

**Shukrani** ........................................ **ii**

**Malengo** ........................................ **iii**

**Maelezo ya Jumla Kuhusu Ratiba** ........................................ **1**

**Siku ya 1: Kutafakari ili kuibua maendeleo na changamoto** ........................................ **2**

Somo la 1: Kujitambulisha/Itifaki ........................................ 2

Somo la 2: Kuchunguza zana zilizofaraguliwa (dakika 120) ........................................ 3

Kiambatisho cha 1: Fomu ya Kuchunguza Zana Zilizofaraguliwa ........................................ 4

Somo la 3: Maonesho kwa ajili ya mrejesho ........................................ 5

Somo la 4: Maendeleo na changamoto – Kutembelea maonesho ........................................ 6

Somo la Kufunga ........................................ 6

**Siku ya 2: Kuchunguza mikakati na mbinu mpya** ........................................ **7**

Somo la 5: Mikakati wakati wa kusoma ........................................ 7

Kiambatisho 2: Mkakati mpya 1: Maneno muhimu ........................................ 8

Somo la 6: Mkakati wa kuandika kilichosomwa ........................................ 9

Kiambatisho 3: Mkakati mpya 2: Mazungumzo Mgahawani ........................................ 9

Somo la 7: Mkakati wa msamiati (Dakika 120 hours) ........................................ 11

Kiambatisho 4: Mkakati mpya 3: Kamusi binafsi ........................................ 11

Msamiati /baada ya kusoma ........................................ 11

**Siku ya 3: Kuanda na kutumia matini** ........................................ **13**

Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji ........................................ 13

**Kiambatisho 5: Kuandika matini ya ngazi husika** ........................................ **15**

Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji ........................................ 15

Somo la 9: Matini + mikakati = ufundishaji ........................................ 16

**Kiambatisho 6: Mfano wa andalio la somo la kujifunza kusoma** ........................................ **17**

Somo la 9: Matini + mikakati = ufundishaji ........................................ 17

Kufunga: Kuweka na kushirikisha malengo ........................................ 18

## Maelezo ya Jumla Kuhusu Ratiba

| | |
|---|---|
| **Siku ya 1: Kutafakari ili kuibua maendeleo na changamoto** | |
| Kujisajili | 8:00 – 8:30 |
| Somo la 1: Kujitambulisha/Itifaki | 8:30 – 9:30 |
| Somo la 2: Kuchunguza zana zilizofaraguliwa | 9:30 – 10:30 |
| **Mapumziko ya Chai/Kahawa** | **10:30 – 11:00** |
| Somo la 2: Kuchunguza zana zilizofaraguliwa | 11:00 – 12:00 |
| Somo la 3: Maonesho kwa ajili ya mrejesho | 12:00 – 1:00 |
| **Chakula cha mchana** | **1:00 – 2:00** |
| Somo la 3: Maonesho kwa ajili ya mrejesho | 2:00 – 2:30 |
| Somo la 4: Maendeleo na changamoto | 2:30 – 3:30 |
| Kufunga Siku: Mapitio ya siku ya 2 | 3:30 – 4:00 |
| **Siku ya 2: Kuchunguza mikakati na mbinu mpya** | |
| Somo la 5: Mikakati wakati wa kusoma | 8:30 – 10:30 |
| **Mapumziko ya Chai/Kahawa** | 10:30 – 11:00 |
| Somo la 6: Mikakati ya kuandika kinachosomwa | 11:00 – 1:00 |
| **Chakula cha mchana** | 1:00 – 2:00 |
| Somo la 7: Mikakati ya msamiati | 2:00 – 3:30 |
| Kufunga Siku: Mapitio ya siku ya 3 | 3:30 – 4:00 |
| **Siku ya 3: Kundaa na kutumia matini** | |
| Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji | 8:30 – 10:30 |
| **Mapumziko ya Chai/Kahawa** | 10:30 – 11:00 |
| Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji | 11:00 – 12:00 |
| Somo la 9: Matini + mkakati = ufundishaji | 12:00 – 1:00 |
| **Chakula cha mchana** | 1:00 – 2:00 |
| Somo la 9: Matini + mkakati = ufundishaji | 2:00 – 3:00 |
| Kuweka na kushirikishana malengo | 3:00 – 4:00 |
| Kufunga: Kutathmini mafunzo | 4:00 – 4:30 |

**Vifaa:**

1. Kalamu.
2. Daftari.
3. Projekta, kompyuta.
4. Chati ya karatasi/bango kitita na standi yake.
5. Kalamu za wino mzito/maka peni.
6. Kadi za sentensi.
7. Vikaratasi vyenye gundi vya kubandika.
8. Fomu za kujisajili, Ratiba, fomu ya kuchunguza zana zilifaraguliwa, karatasi za mikakati mpya, fomu ya andalio la somo, na fomu ya tatimini.

## Siku ya 1: Kutafakari ili kuibua maendeleo na changamoto

**Somo la 1: Kujitambulisha/Itifaki** (dakika 60)

**Vifaa:** Ratiba, daftari la kuandikia, kalamu, chati ya karatsi/bango kitita, kalamu za wino mzito/maka peni, vikaratasi vyenye gundi vya kubandika

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 15 | Kutambulisha mafunzo:<br>1. Malengo<br>2. Kupitia ratiba ya siku tatu<br>3. Itifaki | Kusikiliza na kushiriki |
| Dakika 15 | Kutambulisha washiriki wa mafunzo:<br>1. Wawezeshaji<br>2. Washiriki<br>3. Wageni | |
| Dakika 30 | Kuwezesha mchakato wa washiriki kujiwekea malengo ya mafunzo:<br>1. Kutafakari na kuandika kwa haraka<br>2. Majadiliano katika vikundi<br>3. Majadiliano katika kundi zima<br>4. Andika kwa kifupi malengo ya kundi zima na kuyabandika ukutani (chati moja) | Kutafakari maswali haya kwa kujibu na kuandika kwa haraka:<br>***1. Malengo yako ni yapi kwa siku hizi tatu za mafunzo?***<br>***2. Unatarajia kujifunza na kufanya kitu gani zaidi?***<br>Kujadili majibu yao katika vikundi na kuwasilisha malengo waliyokubaliana katika kikundi chao kwenye kundi zima. (*yasizidi manne*) |

**Somo la 2: Kuchunguza zana zilizofaraguliwa (dakika 120)**

**Vifaa:** daftari la kuandikia, kalamu, chati ya karatsi/bango kitita, kalamu za wino mzito/maka peni, vikaratasi vyenye gundi vya kubandika, zana zilizofaraguliwa, na fomu ya kuchunguza zana.

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 15 | Kuandaa mchakato wa kuchunguza zana zilizofaraguliwa | Kuuliza maswali na ufafanuzi |
| Dakika 60 | Kuwezesha mchakato wa kuchunguza zana za kufundishia zilizofaraguliwa.<br><br>Andika kwenye chati maelekezo haya na kuyabandika ukutani:<br><br>1. *Tandaza aina ya zana zako za kufundishia kwenye meza*<br>2. *Chunguza aina ya zana zako kwa kutumia maswali yaliyoko katika fomu ya kuchunguza zana ulizofaragua*<br>3. *Jadilianeni kwenye vikundi*<br>4. *Andikeni mbinu za kufundishia zinazofanana na zile za kipekee zilizojitokeza* | Kutafakari na kupitia zana zao za kufundishia walizozitandaza kwenye meza kwa kujibu maswali yaliyopo katika fomu ya kuchunguza zana zilizofaraguliwa<br><br>Kushirikishana majibu yao walivyojibu katika fomu na kujadiliana katika kikundi<br><br>Kutumia fomu kubaini na kuandika kufanana na kutofautiana kwa mbinu za kila mshiriki wakati wa majadiliano<br><br>Kutengeneza chati ya T na kuitumia kuandika mbinu zinazofana na za kipekee zilizojadiliwa<br><br>Mchakato huu utawafanya walimu kupitia ufundishaji wao na kubaini njia wanazotumia ambazo mbinu zake ni zilezile/zinafanana au ni tofauti |
| Dakika 30 | Kuwezesha mchakato wa vikundi kuwasilisha kwa kifupi walichoandika kwenye chati yao ya T na kubandika ukutani | Kuchagua mwalimu mmoja katika kikundi kuwasilisha mbinu zao za ufundishaji (zinazofanana na zile za kipekee) |
| Dakika15 | Kuwaelekeza walimu kubandika chati ya T karibu na meza waliyotandaza zana zao. | Kuweka zana zao za kufundishia karibu na chati yao waliyowasilisha katika kundi zima. |

## Kiambatisho cha 1: Fomu ya Kuchunguza Zana Zilizofaraguliwa

**Somo la 2: Kuchunguza zana zilizofaraguliwa**

| Maswali ya Kutafakari | Andika majibu kwa haraka |
|---|---|
| Lengo lako la kufundisha lilikuwa ni nini? Ulitaka wanafunzi wajifunze nini? | |
| Uliamuaje mikakati ya kufundishia utakayoitumia? | |
| Uliamuaje rasilimali/vifaa utakavyovitumia? | |
| Ni mchakato gani ulioutumia kufundisha? | |
| Mwitikio wa wanafunzi ulikuwaje wakati wa ufundishaji? | |
| Ni kwa kiasi gani somo limesaidia wanafunzi kujifunza ulichopanga kufundisha? | |
| Ulijuaje kama somo lako limefanikiwa ama la? | |
| Unawezaje hapo baadaye kufundisha somo hili tofauti? | |
| **Njia za zinazofanana za kufundisha somo** | **Njia za kipekee za kufundisha somo** |
| | |

**Somo la 3: Maonesho kwa ajili ya mrejesho** (Dakika 90)

**Vifaa:** Daftari la kuandikia, kalamu, chati ya karatsi/bango kitita, kalamu za wino mzito/maka peni, vikaratasi vyenye gundi vya kubandika

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 15 | Kuandaa na kuwezesha kipindi cha vikundi kufanya mazoezi na kutoa mrejesho | Kuuliza maswali yoyote waliyonayo kuhusu mchakato wa kipindi hiki |
| Dakika 60 | Kufuatilia na kutoa msaada unaohitajika | Kutafakari kuhusu somo lililopita la zana faraguzi za kufundishia<br><br>Kila kikundi kichague walimu watatu (walimu wanaweza kujitolea) watakaoonesha mfano wa kufundisha masomo wanayofundisha wanafunzi wao. Walimu wengine katika kikundi washiriki kama wanafunzi wanaofundishwa kisha baadaye watoe mrejesho kwa mwalimu aliyeonesha mfano wa kufundisha somo kwa kuonyesha mambo **chanya** aliyofanya na pia **wangependa** afanye nini zaidi. (walimu watoe mrejesho wa mambo mazuri aliyofanya mwalimu na pia jambo ambalo wangependa mwalimu alifanye ili somo liwe zuri zaidi atakapolifundisha tena) |
| Dakika 15 | Kuwezesha mchakato wa mrejesho wa kundi zima kupitia mazoezi ya kufundisha waliyofanya walimu:<br><br>1. *Ni kitu gani umeona walimu wakikifanya vizuri katika kikundi chenu?*<br>2. *Umejifunza nini katika mazoezi haya ya kufundisha waliyofanya walimu?*<br>3. *Utatumiaje mazoezi haya kukusaidia kufundisha vizuri zaidi darasa lako?* | Kushiriki katika majadiliano ya kupitia mazoezi yaliyofanywa na walimu. |

**Somo la 4: Maendeleo na changamoto – Kutembelea maonesho** (Dakika 60)

**Vifaa:** Daftari la kuandikia, kalamu, vikaratasi vyenye gundi vya kubandika

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 20 | Kuwezesha mchakato wa kutafakari | Kurejea walichofanya siku nzima na kujibu kwa kuandika haraka majibu ya swali hili:<br><br>***Ni kitu gani umeona leo kinakuchofanya ujue kuwa kuna maendeleo katika ufundishaji wako na ufundishaji wa walimu wenzako?*** |
| Dakika 20 | Kuwezesha mchakato wa matembezi kuangalia kazi za walimu | Kutembea katika chumba na kuchunguza chati za T walizobandika ukutani na vifaa faraguzi vya kufundishia walivyotandaza walimu. Walimu watumie karatasi ndogo za rangi zenye gundi kutoa mrejesho chanya na mapendekezo yao kuhusu zana faraguzi za walimu. Watumie karatasi zenye rangi tofauti kama ifuatavyo:<br>**Rangi ya 1:** Kutoa mrejesho chanya kwa zana za walimu wenzao<br>**Rangi ya 2:** Kutoa mapendekezo ya kuboresha zaidi |
| Dakika 20 | Kuwezesha mchakato wa kufanya majumuisho | Kila mwalimu arudi kwenye kazi na zana zake na kusoma mrejesho na mapendekezo ya kuboresha yaliyotolewa na walimu wenzake. Baadaye arudi kwenye meza ya kundi lake na kujadili mrejesho waliopewa. |

**Somo la Kufunga** (Dakika 30)

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| **Dakika 30 Kutafakari** | Waongoze walimu kuangalia malengo waliyojiwekea asubuhi na kuyajadili.<br><br>*Ni malengo yapi katika yale yaliyoandikwa yamefikiwa?*<br>Kueleza kwa ufupi siku ya pili ratiba itakuwa na mada gani? | Kupitia tena malengo ya mafunzo na kujadiliana ili kubaini malengo yaliyofikiwa. |

## Siku ya 2: Kuchunguza mikakati na mbinu mpya

**Somo la 5: Mikakati wakati wa kusoma** (Dakika 120)

**Vifaa:** Viambatanisho vya mikakati mipya ya kusoma (Viko katika Mwongozo huu)

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| **Dakika 45**<br><br>**Kabla ya kusoma** | Waongoze walimu katika majadiliano kwa kutumia maduara ya Sokratesi ili kubaini ni mikakati gani wanayotumia wakati wa *kusoma ili kujifunza* darasani. | Kushiriki katika majadiliano:<br>- *Ni mikakati gani ya* ***kusoma ili kujifunza*** *unayotumia mara kwa mara darasani wakati wanafunzi wanasoma? Kwa nini?*<br>- *Kuwa na shughuli maalum wakati wa kusoma kunamsaidiaje mwanafunzi kujifunza maudhui ya somo? Unajuaje?* |
| **Dakika 60**<br><br>**Wakati wa kusoma** | Kuonesha mkakati mmoja mpya wa kusoma ili kujifunza pamoja na walimu kwa kutumia matini mojawapo inayotumika darasani.<br><br>Kujibu maswali na kufafanua jambo lolote walilotatizwa nalo.<br><br>Waoneshe Kiambatisho cha mkakati mpya ndani ya Mwongozo huu na kuupitia pamoja. | Walimu washiriki katika somo la mfano. Waulize maswali waliyonayo yanayohitaji ufafanuzi zaidi.<br><br>Wapite na kuchunguza mkakati mpya kama ulivyooneshwa katika mwongozo. |
| **Dakika15**<br><br>**Baada ya kusoma** | Waongoze walimu kuandika kwa haraka jinsi watakavyotumia mkakati huu mpya katika ufundishaji wao.<br><br>Wawasilishe walichoandika katika kundi zima. | Kuandika jinsi watakavyotumia mkakati huu mpya na kuwasilisha katika kundi zima. |

## Kiambatisho 2: Mkakati mpya 1: Maneno muhimu

**Somo la 5: Wakati na Baada ya kusoma/msamiati**

**Maelezo:** Maneno muhimu ni mbinu ya wakati wa kusoma ambayo inamsaidia mwanafunzi kubainisha mawazo makuu, maudhui muhimu na msamiati muhimu wakati akiwa anasoma. Mwanafunzi anatumia penseli wakati akisoma kuzungushia neno muhimu moja katika kila sentensi linalotoa muhtasari mzuri wa taarifa muhimu katika sentensi hiyo.

**Matokeo ya Kujifunza:** Wanafunzi waweze:

1. Kutofautisha kati ya taarifa muhimu na zile zisizo za muhimuy
2. Kubainisha msamiati muhimu kutokana na matini wanayosoma
3. Kujadili maudhui/dhana na msamiati kwa ufahamu

**Vifaa:** Matini, Kalamu/penseli

**Hatua:**

1 Mwanafunzi anasoma matini wakti huo huo akizungushia neno muhimu moja katika kila sentensi linalotoa muhtasari mzuri wa taarifa muhimu katika sentensi hiyo.

2 Baada ya kusoma, mwalimu na wanafunzi wanajadili
Ni maneno gani muhimu yamezungushiwa? Kwa nini umezungushia maneno hayo?
Kuna mwanafunzi yoyote aliye zungushia maneno mengine ambayo wenzake hawakuyazungushia? kwa nini?

**Muunganiko:** Baada ya kutumia mbinu hii, mwalimu anaweza kufuatilia kwa kuwataka wanafunzi kuyaweka yale maneno muhimu zaidi katika kamuzi zao binafsi kwa ajili ya kuyatumia na kujifunza.

**Upimaji usiorasmi:** Mwalimu achunguze kiwango gani wanafunzi wamefikia katika kubainisha maneno muhimu katika matini.
Kubainisha maneno muhimu kuonaonyesha a) uwezo wa kuielewa matini, b)kuelewa msamiati; c) kuelewa dhana muhimu katika maudhui.

**Somo la 6: Mkakati wa kuandika kilichosomwa** (Dakika 120)

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| **Dakika 45**<br><br>**Kabla** | Waongoze walimu katika majadiliano kwa kutumia maduara ya Sokratesi ili kubaini ni mikakati gani wanayotumia inayohusisha ***kuandika*** kama mchakato wa kutafakari. | Kushiriki katika majadiliano:<br>1. *Ni mikakati gani ya kusoma unayotumia kwa sasa ambayo inahitaji wanafunzi **waandike** wanapokuwa wanatafakari walichokisoma?*<br><br>2. *Je kuandika kunawasaidiaje wanafunzi kuelewa vizuri zaidi kile walichosoma?* |
| **Dakika 60**<br>**Wakati** | Kuonesha mfano pamoja na walimu, mkakati mmoja mpya wa kuandika ili kujifunza, kwa kutumia maudhui ya darasani<br><br>Kujibu maswali ya walimu<br><br>Wape/waoneshe walimu Kiambatisho cha mkakati mpya ili waupitie (mazungumzo mgahawani) | Walimu washiriki katika somo la kuonesha mfano. Waulize maswali waliyonayo. Wapitie Kiambatisho chenye mkakati mpya(mazungumzo mgahawani) |
| **Dakika 15**<br>**Baada** | Waombe walimu watengeneze mkanda wa sentensi kuelezea jinsi gani watatumia angalau mkakati moja mpya katika kufundisha.<br><br>Wabandike sentensi hizo ukutani. | Walimu watengeneze mikanda ya sentensi na kuzibandika ukutani. |

**Kiambatisho 3: Mkakati mpya 2: Mazungumzo Mgahawani**

**Somo la 6: Mkakati wa kuandika kilichosomwa**

**Baada ya kusoma**

**Maelezo:** Mazungumzo mgahawani ni mchakato wa majadiliano ya baada ya kusoma, ambapo mwalimu anawapatia maswali muhimu wanafunzi katika vikundi vidogo kuhusu matini (kila swali liwe katika karatasi moja). Wanafunzi wanafanya kazi katika vikundi vidogo kuandika majibu yao kama kikundi. Wakimaliza wanawapatia kikundi kingine karatasi yenye swali walilomaliza kujibu. Vikundi vyote vinajibu maswali yote kwa kuandika na baadaye wanarejesha karatsi zote za

majibu kwenye kikundi cha kwanza kwa ajili ya kupitia mara ya mwisho na kufanya muhtasari na majadiliano.

**Matokeo ya kujifunza:** Wanafunzi wataweza

1. Kujadili maudhui na dhana muhimu kutokana na matini waliyosoma
2. Kuandika mawazo yao kuhusu maudhui na dhana kutokana na matini waliyosoma
3. Kushirikiana katika kuchangia mawazo
4. Kuunganisha mawazo ya wengine

**Vifaa:** Karatasi, kalamu/penseli

**Hatua:**

1 Wanafunzi wanasoma matini kwanza

2 Mwalimu anawapatia wanafunzi maswali ya kujibu katika vikundi vidogo kuhusu matini waliyomaliza kusoma. Vikundi visiwe vikubwa zaidi ya wanafunzi wanne. Maswali yatokane na matini na maudhui waliyosoma na idadi yake iwe sawa na vikundi. Maswali yawe ni ya ngazi ya juu, yanayowafanya wanafunzi kufukiri, kujadili na kuandika majibu yenye upeo wa juu. (maswali ya ndiyo na hapana hayatakiwi katika mchakato huu)

3 Mchakato katika vikundi: Mwanafunzi mmoja anasoma swali kwa sauti. Wanafunzi katika kikundi wanajadiliana kuhusu swali hilo na majibu yake. Wanafunzi waamua kwa pamoja nini cha kuandika kwenye karatasi.

4 Karatasi za maswali wanapewa kikundi kingine na mchakato wa kujibu unaendelea kama walivyofanya kikundi cha kwanza. Rudia mchakato huu mpaka vikundi vyote vijibu maswali yote.

5 Baada ya vikundi vyote kujibu maswali yote, karatasi zenye majibu zinarudishwa kwenye kikundi cha kwanza. Kikundi hiki kinasoma majibu yote yaliyoandikwa kwenye karatasi kwa sauti. Baadaye wanaamua kwa pamoja kuandika kwa muhtasari majibu yote waliyosoma.

6 Darasa zima linajadili kwa kifupi majibu ya kila swali.

**Upimaji usiorasmi:** Mwalimu atakusanya karatsi za majibu na kuzipitia ili kujua kile walichojifunza wanafunzi. Mwalimu atasikiliza na kufukiri kuhusu mihtasari ya majibu yaliyotolewa katika vikundi wakati wa mijadala ya majumuisho ili kujua ni kwa kiasi gani wanafunzi wamefanya vizuri kutoa mihtasari ya mambo muhimu kuhusu maudhui katika matini waliyosoma.

## Somo la 7: Mkakati wa msamiati (Dakika 120 hours)

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| **Dakika 45** | Waongoze walimu katika maduara ya Sokratesi kujadili kuhusu mikakati ya kufundisha msamiati wanayotumia kwa sasa darasani | Washiriki katika majadiliano:<br>1. *Ni mikakati ipi ya kufundisha msamiati unayotumia zaidi darasani? kwa nini?*<br>2. *Ni kwa namna gani kazi ya kujifunza msamiati humsaidia mwanafunzi kujifunza maudhui ya somo? Unajuaje?* |
| **Dakika 60** | Kuonesha mfano pamoja na walimu, mkakati mmoja mpya wa kufundisha msamiati kwa kutumia mfano wa maudhui ya somo darasani<br><br>Kujibu maswali ya walimu<br><br>Wape/waoneshe walimu Kiambatisho cha mkakati mpya ili waipitie (kamusi binafsi) | Walimu washiriki katika somo la kuonesha mfano. Waulize maswali waliyonayo. Wapitie Kiambatisho Chenye mkakati mpya (kamusi binafsi) |
| **Dakika15** | Waombe walimu kufikiria kuhusu maudhui wanayofundisha na waandike msamiati muhimu wanaoweza kuufundisha kwa kutumia mbinu mpya ya msamiati.<br><br>Waambie washirikishane katika vikundi vyao. | Walimu kubaini msamiati muhimu na kushirikishana katika vikundi vyao |

## Kiambatisho 4: Mkakati mpya 3: Kamusi binafsi

**Somo la 7: Mkakati wa msamiati**

**Msamiati /baada ya kusoma**

**Maelezo:** Kamusi za binafsi ni sehemu ya daftari la mazoezi la mwanafunzi, ambapo wanaweka msamiati mpya kwa kadri wanavyoendelea kujifunza darasani. Siyo kwamba ni orodha ya maelezo ya maana za maneno yatolewayo na mwalimu, isipokuwa ni jedwali la pande nne ambapo mwanafunzi:

1.Mwanafunzi anaandika neno
2. Mwanafufunzi mwenyewe anaandika maelezo ya maana ya neno

3. Mwanafunzi anatumia neno katika sentensi yenye maana (iliyotungwa na mwanafunzi mwenyewe)
4. Mwanafunzi anachora picha rahisi itakayomsaidia kulikumbuka neno na maana yake

**Matokeo ya Kujifunza:** Wanafunzi wataweza

1. Kubainisha dhana muhimu na msamiati unaotokana na maudhui mahsusi ya mada
2. Kutengeneza maelezo yao wenyewe ya maana muhimu za msamiati wa maudhui
3. Kuelewa jinsi ya kuzungumza na kuandika kuhusu maudhui waliyojifunza
4. Kutengeneza maelezo yao wenyewe ya kuwakumbusha (vielelezo vya picha)

**Vifaa:** Madaftari ya mazoezi ya wanafunzi, kalamu na penseli

**Hatua:**

1 Mwalimu na wanafunzi wanabungua bongo kuhusu msamiati muhimu waliojifunza wakati wa somo, na kuandika maneno hayo kwenye ubao

2 Wanafunzi wanatumia jedwali la pande nne kukamilisha kamusi zao binafsi

**Upimaji usiorasmi:** Mwalimu anaweza kukusanya na kupitia kamusi binafsi za wanafunzi na kuchunguza ni kwa jinsi gani wanafunzi wanakamilisha kamusi zao binafsi. Mwalimu anaweza kuwafanya wanafunzi washiriki katika majadiliano darasani kuhusu maudhui muhimu na msamiati wake.

**Mfano:**

| | |
|---|---|
| **Wingu** | **ni kama fungu la pamba angani lenye mvuke** |
| **Wingu ni jeupe nene, na limebeba mvua** |  |

## Siku ya 3: Kuanda na kutumia matini

**Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji** (Dakika 180)

**Vifaa:** Vitabu (kila kikundi kiwe na angalau kitabu kimoja), matini za ngazi mbalimbali za usomaji, daftari la kuandikia, kalamu na vifaa vya kutengenezea vitabu.

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 45 | Tambulisha dhana ya matini inayoendana na ngazi ya usomaji, kwa kujadili taarifa ifuatayo:<br><br>*Matini inayoendana na ngazi ya usomaji ni ile matini iliyochaguliwa kulingana na kiwango cha uwezo wa kusoma cha mwanafunzi. Siyo matini rahisi sana au ngumu kwa mwanafunzi kuisoma. Mwanafunzi wakati akiisoma matini hii anapata changamato lakini anamudu kuisoma na kuelewa alichosoma. Matini ya kusoma wakati wa kufundishwa siyo sawa na matini ya kusoma mwenyewe kwa kujitegemea. Matini ya kufundishia lazima ilete changamoto kwa mwanafunzi, na matini ya kusoma mwenyewe kwa kujitegemea lazima iwe rahisi kusoma.*<br><br>Washirikishe kuipitia na kusoma Kiambatisho chenye maelezo kuhusu matini inayoendana na ngazi ya usomaji<br><br>Waambie waandike mambo muhimu na kama wana maswali.<br><br>Kujadili mambo muhimu na kujibu maswali yaliyojitokeza | Waandike maelezo kuhusu maana ya matini inayoendana na ngazi ya usomaji katika madaftari yao.<br><br>Wasome na kupitia Kiambatisho kinachoelezea matinini inayoendana na ngazi ya usomaji.<br><br>Waandike mambo muhimu na maswali yanayojitokeza<br><br>Wajadiliane mambo muhimu na maswali yaliyojitokeza katika vikundi vyao. |
| Dakika 20 | Wezesha mazoezi ya kufundisha (katika vikundi). Bandika maswali yafuatayo:<br>1. *Ni ngazi ipi ya kitabu* | Wafanye kazi katika vikundi kuchunguza vitabu vilivyotolewa na TZ21. Watumie maelezo yaliyo kwenye Kiambatisho cha matini |

| | | |
|---|---|---|
| | *unachokipita sasa? Unajuaje?*<br>2. *Wanafunzi gani unadhani watafaidika zaidi kwa kutumia kitabu hiki wakati wa somo kusoma kwa usadizi wa mwalimu: ni darasa la 1 au la 2?*<br>3. *Ni wanafunzi gani wataweza kusoma kitabu hiki wenyewe bila msaada wa mwalimu? Unajuaje?* | inayoendana na ngazi ya usomaji na kujadiliana ngazi ya kitabu hicho.<br><br>Walimu watafakari na kujibu maswali haya matatu na kuandika mambo muhimu kwenye madaftari yao. |
| Dakika 15 | Waongoze walimu kujadili  ugumu wanaoupata kuhusu wanafunzi wa darasa la 3 na la 4 kuwa tayari kusoma matini inayowahusu:<br>1. *Baadhi ya wanafunzi hawako tayari kabisa kusoma matini inayotolewa kwa maudhui ya darasa la 3 na la 4.*<br>2. *Baadhi ya wanafunzi wako tayari kabisa na wala hawapati changamoto yoyote kusoma matini inayotolewa.*<br>3. *Ni lazima walimu watoe matini rahisi, matini inayoendana na ngazi ya usomaji na matini iliyo juu ya ngazi ya usomaji*<br>4. *Matini hizi zinasaidia na kutoa changamoto ya usomaji kwa wanafunzi waliotayari katika ngazi mbalimbali* | Walimu waandike mambo muhimu |
| Dakika 80 | Waongoze walimu katika mchakato wa kuandika vitabu. Hakikisha kuwa matini ya ngazi ya chini, ngazi ya kati na ngazi ya juu zimegawiwa kwa uwiano sawa katika mchakato wa kuziandika. Bandika ukutani yafuatayo ili kuwakumbusha walimu:<br><br>*1.Fikiria mada inayofuata toka katika mhutasari utakayoifundisha darasani. Tayarisha matini leo utakayotumia kufundisha darasani.*<br>*2.Tumia Kiambatisho cha* ***Matini*** | Walimu wafanye kazi katika jozi kuandika vitabu vifupi kutokan na maudhui ya somo lao. Jozi lazima zichague au zigawiwe kuandika vitabu vya 1) ngazi ya chini, 2) vitabu vya ngazi ya kati (vinavyotumika kufundishia/kusoma kwa usaidizi wa mwalimu), 3) vitabu vya ngazi ya juu. |

| | | |
|---|---|---|
| | ***inayoendana na ngazi ya usomaji*** *kutayarisha kitabu kitakachowafaa wanafunzi unaowalenga/unaowafundisha (ngazi ya chini, ngazi ya kati, ngazi ya juu).*<br>*3. Andika kitabu kifupi kitakachowavutia wanafunzi wako chenye maudhui muhimu.*<br>*4. Wakati unaandika kitabu, fikiria jinsi utakavyokitumia na wanafunzi wako.* | |
| Dakika 30 | Kuongoza mchakato wa kushirikishana kile walimu walichotayarisha na kupeana mrejesho | Kila jozi za walimu zishirikishane na kupeana mrejesho wa vitabu vipya walivyoandaa. Wasome kwa sauti maudhui ya vitabu vyao na kujadili kuhusu ngazi inayohusika, jinsi kitabu kitakavyovutia na jinsi watakavyotumia kitabu hicho darasani. |

## Kiambatisho 5: Kuandika matini ya ngazi husika

**Somo la 8: Matini inayoendana na ngazi ya msomaji**

**Maelezo:** Kuchagua matini sahihi ya kufundishia kusoma ni muhimu kama zilivyo muhimu shughuli zingine anazopanga mwalimu. Ni muhimu kufikiria matini ya kufundishia katika makundi matatu:

**Ngazi ya Kufundishia:** Matini ya kundi hili inafaa kufundishia wanafunzi wakati wanapojifunza, wanaweza kujua takiribani msamiati unaotumika, ingawa siyo maneno yote. Urefu wa matini ni ule unaofaa kulingana na umri wao na mada wanazosoma in zile zinazowavutia. Matini haya ni **ya ngazi ya kati.**

**Ngazi za kujitegemea:** Matini katika kundi hili inafaa kwa wanafunzi kusoma wao wenyewe kwa kujifurahisha. Matini katika ngazi hii iko katika **ngazi ya chini** zaidi kuliko ile ya ngazi ya kufundishia. Hii ni kwa sababu wanafunzi lazima waweze kuisoma matini hiyo bila kufundishwa au kuhitaji usaidizi wa mwalimu.

**Ngazi ya kuhangaisha:** Matini ya kundi hili ni ya **ngazi ya juu sana** kwa wanafunzi kuisoma katika mazingira yoyote yale. Matini katika kundi hili kamwe yasitumike kwa kufundishia au kwa wanafunzi kusoma wenyewe na wala yasiwepo katika mazingira ya darasani.

| Darasa | Ngazi ya maudhui ya kusoma |
|---|---|
| Darasa la 2 | • Maneno na sentensi zenye herufi kubwa<br>• Alama za msingi za uandishi<br>• Herufi muambatano<br>• Sentensi rahisi (bila alama ya mkato)<br>• Matini fupi zenye maneno kati ya 50 na 100 |
| Darasa la 3 | • Maneno na sentensi zenye herufi kubwa<br>• Majina ya pekee<br>• Alama ngumu za uandishi<br>• Sentensi ngumu<br>• Matini fupi (za taarifa na kubuni) maneno kati ya 50 – 150<br>• Aya fupi (zenye sentensi 2-4)<br>• Michoro na chati rahisi |
| Darasa la 4 | • Maneno na sentensi zenye herufi kubwa<br>• Majina ya pekee<br>• Alama ngumu za uandishi<br>• Sentensi ngumu<br>• Aya ndefu (zenye sentensi kati ya 5-7)<br>• Matini ndefu (za taarifa na kubuni) kati ya maneno 100 – 200<br>• Michoro na chati ngumu |

## **Somo la 9: Matini + mikakati = ufundishaji** (Dakika 120)

**Vifaa:** Vifaa vyote na maudhui yaliyotumika tangu siku ya 1, 2 and 3

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| Dakika 15 | Waombe walimu kufikiria kuhusu maudhui mahsusi yanayowasilishwa na vitabu/matini waliyotayarisha (hapo juu). Waandike kuhusu:<br>1. *Msamiati muhimu ambao lazima wanafunzi wautambue.*<br>2. *Mawazo makuu ya maudhui ambayo lazima wanafunzi wajifunze.*<br>3. *Namna gani matini itasaidia kujifunza hayo.* | Walimu watafakari na kuandika |
| Dakika 60 | Waambie walimu kuandaa somo ambalo litatumia matini/kitabu walichoandika. Waambie wabainisha yafuatayo:<br>1. *Msamiati muhimu wa somo*<br>2. *Mikakati ya kusoma, kuandika na/au msamiati watakayotumia.*<br>3. *Matokeo wanayoyatarajia kutokea kwa* | Walimu kukamilisha mchakato wa kuandaa somo kwa kutumia matini/kitabu walichoandika. |

| | | |
|---|---|---|
| | *wanafunzi.* | |
| Dakika 45 | Waombe walimu kutengeneza jozi (jozi mpya) na washirikishane somo waliloandaa na jinsi watavyotumia matini/kitabu walichoandika.<br>Waombe wapeane mrejesho wenye manufaa kila moja kwa kile alichokifanya. | Walimu watengeneze jozi mpya na kushirikishana somo waliloandaa na matini watakayotumia.<br><br>Wasikilize na kukubaliana na mrejesho watakaopewa na wenzao. |

## Kiambatisho 6: Mfano wa andalio la somo la kujifunza kusoma

**Somo la 9: Matini + mikakati = ufundishaji**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya somo** | |
| **Maudhui ya somo** | |
| **Msamiati muhimu** | |
| **Kichwa cha habari cha matini** | |
| **Ngazi ya matini** | |
| **Ufupisho wa matini (muhtasari)** | |
| **Mbinu za kabla ya kusoma** | |
| **Mbinu za wakati wa kusoma** | |
| **Mbinu za baada ya kusoma** | |
| **Mbinu za upimaji** | |

**Kufunga: Kuweka na kushirikisha malengo** (dakika 60)

| Muda | Shughuli ya Mwezeshaji | Shughuli za Mwalimu |
|---|---|---|
| **Dakika 20**<br><br>**Kabla** | Waambie walimu kutafakari kuhusu malengo ya mafunzo waliyojiwekea siku ya kwanza.<br><br>Waambie kubainisha malengo yaliyofikiwa na yale ambayo hayakufikiwa wakati wa mafunzo haya. Wajadili kwa nini mafunzo yamefikia malengo fulani na malengo mengine hayakufikwa? Watoe mapendekezo jinsi walimu watavyoendelea kufanya kazi ili kufikia yale malengo ambayo hayakufikiwa katika mafunzo. | Kutafakari malengo ya mafunzo na kubaini yale yaliyofikiwa na yale ambayo hayakufikiwa |
| **Dakika 30**<br><br>**Wakati** | Kuwaambia walimu waweka malengo mawili mahsusi kwa ajili yao wenyewe na kuhusu kufundisha<br><br>Waambie wayaandike malengo haya mahsusi mawili kwa ajili yao wenyewe na kuhusu ufundishaji (nakala 2). Washirikishane malengo yao katika vikundi. Kisha kusanya nakala moja ya malengo ya kila mwalimu. | Walimu kuweka malengo mawili mahsusi na kuyaandika kwenye karatasi (nakala 2). Washirikishane malengo yao katika vikundi. Nakala moja wamkabidhi mkufunzi na nakala nyingine waondoke nayo. |
| **Dakika 10** | Waambie wajaze fomu ya tathmini ya mafunzo | Kujaza fomu ya tathmini. |